# MIAKA 500 YA MATENGENEZO YA KANISA NA USHUHUDA WETU

Na Askofu Dr. Abednego Keshomshahara

## 1. UTANGULIZI

Miaka 500 ya matengenezo ya Kanisa inatufanya tuangalie nyuma na kuona jinsi Mungu alivyotumia wanadamu kurekebisha na kutengeneza kanisa lake liweze kufanya kazi yake ya msingi ambayo ni ujumbe wa kuokolewa kwa Neema tu kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo. Matengenezo ya kanisa yanatukumbusha kuwa mwanadamu hawezi kuokolewa kwa njia ya matendo ya sheria.

Hata hivyo Mafundisho rasmi ya Kilutheri ya wakati wote na mahali pote huonesha kuwa tunapokelewa jinsi tulivyo lakini hatupaswi kubaki jinsi tulivyopokelewa. Hatua ya kubadilishwa ni ya utakaso. Katika Warumi 6:1 - 4 Mtume Paulo anasema kuwa tunapookolewa kwa neema hatupaswi kuishi katika dhambi bali inabidi tubadilike na kuwa na maisha mapya. Kwa sababu hii, anazidi kusema "ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya" (1Kor. 5: 17).

Kwa miaka mingi tumekazia neema tukasahau utakaso ambapo inabidi imani izae matunda ya imani ambayo yanathibitisha kuokolewa kwetu. Katika Mathayo 7:19 Neno linasema "mti usiozaa matunda utakatwa". Na katika Mathayo 25: 36 - 46 tunaambiwa kuwa siku ya mwisho kigezo cha kurithi uzima au kutorithi uzima ni jinsi tulivyojali na kutendea wengine: kuvika walio uchi, kulisha wenye njaa, kutembelea wagonjwa, walio kifungoni, nk.

Utakaso ni kazi ya Roho Mtakatiu inayotutaka tutubu dhambi, tusamehe dhambi, tuwe na upendo, tujitoe na kutoa mali zetu kwa ajili ya kazi ya Mungu, kumtumikia Bwana, kuomba Mungu na kuzaa matunda ya imani.

Mwanzilishi wa matengenezo ya Kanisa Dkt. Martin Luther alisimamia ukweli wa Neno la Mungu katika kupambana na mafundisho potofu yaliyofanya wokovu ufikie hatua ya kununuliwa kwa hela kupitia vyeti vya msamaha pamoja na mapungufu mengine tutakayoona baadaye.

Kutokana na mchango wake mkubwa katika historia ya kanisa na dunia kwa ujumla, mwanahistoria James Kittelson wa Marekani anasema kuwa katika maktaba kubwa duniani vitabu vilivyoandikwa na Martini Luther na vile vilivyoandikwa juu ya Martin Luther vinachukua nafasi kubwa kuliko binadamu wengine isipokuwa Yesu wa Nazareti. Anaongeza kusema kuwa hata serikali ya kikomunisti iliyoongoza Ujerumani Mashariki ilitoa uzito mkubwa kwenye sherehe ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Martin Luther kuliko siku ya kukumbuka ya miaka 100 ya kufa kwa Karl Marx, mwanzilishi wa itikadi ya Ukomunisti wa Kimaksisti[1].

Martin Luther mwenyewe alikuwa mwandishi wa vitabu vingi juu ya imani. Aliandika zaidi ya vitabu 100 vikubwa. Alikuwa mtu muhimu kiasi cha kutajwa mara kwa mara na maadui zake pamoja na waliompenda. Martin Luther alitaja kuwa wapo waliomuita "muasi mtiifu" na wengine walimuita "shetani wa vichwa saba (7)". Marafiki zake wa karibu walimuita nabii Eliya aliyetumwa na Mungu. Mawazo yake yaliibua hoja na

[1] James M. Kittelson, *Luther the Reformer: The Story of the Man and his Caree*r ( Minneapolis: Fortress Press, 2003), 9.

mivutano mikubwa kitheolojia siku zile na hata siku hizi[2]. Siku ya kufa kwake ilitangazwa ulaya nzima wakati siku alipozaliwa haikuwa na uzito wowote kiasi kwamba yeye na marafiki zake walibishana juu ya tarehe ya kuzaliwa kwake maana haikujulikana wazi[3].

Dkt. Martin Luther alisimama imara bila kumwogopa Papa aliyekuwa na nguvu za kisiasa na kidini akiongoza taasisi iliyomiliki $^{1}/_{3}$ ya ardhi ya ulaya nzima. Tunaweza kusema kuwa Luther alishuhudia ukweli wa Injili kiasi cha kuwa tayari kufa kwa ajili ya ukweli pale aliposema "Hapa nasimamia ukweli wa Neno la Mungu, sitabadili msimamo, nisaidie Mungu wangu". Ni kwa sababu hii, kichwa cha Mada yetu kinaongelea Matengenezo ya miaka 500 kuhusianishwa na Ushuhuda Wetu ambapo inabidi tujihoji kama yanayoendelea siku hizi katikati ya kuibuka kwa madhehebu mengi ya kikarizimatiki yanajengwa kwenye msingi wa Neno la Mungu au la.

Neno kutoka Waefeso 4: 3 linakuwa msingi wa kuhakikisha umoja wa Kanisa la Kilutheri unatunzwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu ili utambulisho wetu udumu ndani ya ushuhuda wetu unaojengwa juu ya Neno, Kristo, Imani na Neema ya Mungu iokoayo.

Ni kwa msingi wa Neno la Mungu tunapaswa kumtumikia Mungu kwa kujitoa na kujituma pamoja na uwepo wa changamoto nyingi za kiuchumi, kijamii na kihistoria. Mtume Paulo anasema kuwa pasiwepo chochote cha kututenga na upendo wa Yesu hata kama ni kiu, uchi, njaa, n.k.

Tunapaswa kulinda mafundisho na umoja wa kanisa bila manung'uniko, malalamiko wala kukatishwa tamaa na jambo lolote. Kama kuna jambo la kurekebisha, tulirekebishe ndani ya kanisa kwa kufuata vikao rasmi ili kazi ya Bwana Yesu isonge mbele. Ni kwa njia hii tutakuwa tumeshinda jaribu analolitaja Mchungaji Buchocho wa Karagwe kuwa Mwanadamu huzaliwa analia, hukua analalamika na kufa bila kuridhika.

Aidha, pamoja na ujumbe wa matengenezo kuleta uhuru wa kukombolewa kiroho, matokeo ya matengenezo yalikuwa makubwa kiasi cha kuleta mabadiliko na mageuzi katika nyanja za siasa, uchumi, sayansi, na jamii. Mageuzi na mabadiliko haya yaligusa mitazamo ya kidini kiasi kwamba mabadiliko yaligusa si tu kanisa la Kirumi bali pia wanamatengenezo wenyewe walifikia hatua ya kutopatana. Walitofautiana kiasi cha kuwa na madhehebu mbalimbali yaliyotokana na wanamatengenezo wenyewe kwa kuwa na mitazamo tofauti ya kibiblia na kitheologia.

Tunaweza kusema kuwa kama matengenezo yasingetokea, dunia ingekuwa na sura nyingine tofauti na ilivyo sasa katika nyanja mbalimbali za maisha. Matengenezo yalifanya wafalme wawe na nguvu kisiasa. Ulaya iligawanyika na kujitegemea bila kutegemea uongozi mmoja wa Roma. Dola takatifu la Roma lilidhoofika. Mfalme Henry wa VIII wa Uingereza alijitenga na Roma baada ya Papa kumzuia kuoa mke wa pili. Alitumia mwanya wa matengenezo kujitenga na Roma na hivyo kuoa mke mwingine na Serikali kuwa na nguvu kuliko kanisa ulaya.

[2] Ibid.
[3] Ibid., 31.

Matengenezo yametokeza sura ya wakristo duniani kuwa na Makanisa ya Kilutheri 144 wanachama wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani. Makanisa haya yana jumla ya wakristo zaidi ya milioni 70 katika nchi 79. Yapo Makanisa ya "reformed" yanayofuata mafundisho ya John Calvin na "Muungano wa Walutheri na "reformed" yenye makanisa 227 na wakristo milioni 80 kwenze nchi 108, na hivyo jumla ya makanisa ya kimatengenezo, yaani walutheri na "reformed" ni zaidi ya milioni 150. Haya ni matokeo ya matengenezo yaliyoanzishwa na Martin Luther (Ujerumani), Kalvin na Zwingli (Uswizi) ambapo baadaye makanisa haya yalisambaa duniani kote[4].

Takwimu zinaonesha kuwa makanisa ya kiprotestanti ambayo hujumuisha makanisa ya matengenezo na makanisa ya kipentekoste na kikarizimatiki yana takribani wakristo bilioni moja[5] ambapo wakatoliki ni bilioni 1.2 na hivyo kuwa na jumla ya wakristo bilioni 2.2 duniani[6]. Makanisa ya kipentekoste na kikarizimatiki yanakua kwa kasi kubwa hasa barani Afrika na Asia Pasifiki. Makanisa ya kipentekoste duniani yana wakristo milioni 279, wengi wao wakiwa barani Afrika. Makanisa ya kikarizimatiki yana wakristo milioni 305 duniani wengi wao wakiwa Asia Pasifiki[7].

Ifahamike kwamba makanisa ya kipentekeoste na kikarizimatiki yalitokana na makanisa ya kimatengenezo. Aidha, makanisa ya kimatengenezo yanajikuta yamezungukwa na madhehebu ya Kikatoliki, Kianglikana, Kiorthodoksi na makanisa ya kipentekoste na Kikarizimatiki[8].

Wapentekoste hukaza kuwa kunena kwa lugha ni alama ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu wakati wakarizimatiki hukaza kuwa ubatizo wa Roho Mtakatifu hutokea pale mtu anapozaliwa mara ya pili kiroho na uthibitisho wake ni karama mbalimbali za Roho Mtakatifu (http://en.m.wikipedia.org/wiki/charismatic).

Ushuhuda wetu ni katikati ya changamoto ya kuhudumu katikati ya madhehebu mbalimbali ambayo huvua wakristo kutoka kwenye makanisa ya kihistoria. Kama Volker Leppin na Dorothea Sattler wanavyoona katika kitabu cha "Reformation 1517-2017: Ökumenische Perspectivien" - maadhimisho ya miaka 500 kwa upande mmoja yanaonesha mafanikio ya matengenezo ya Kanisa lakini kwa upande mwingine yanaonesha umoja wa kanisa ulivyovunjika pakatokea madhehebu mbalimbali duniani.

Tukirudi kwenye idadi ya wakristo duniani kulinganisha na dini nyinigne, mwaka 1910 makanisa ya Ulaya yalidhani yangefanya dunia kuwa ya kikristo ndani ya miaka 25 lakini hali ilivyo mpaka sasa ukuaji wa ukristo haukupatana na ukuaji wa idadi ya wakazi wa dunia.

Kwa sasa wakristo ni $^{1}/_{3}$ ya idadi ya watu duniani, yaani bilioni 2.2 (31%) kati ya watu bilioni 7[9] ambapo waislamu idadi yao ni bilioni 1.6 (23%). Uislamu unaendelea kukua kwa kasi kutokana na mfumo wao wa ndoa za wake wengi pamoja na kuzaa watoto wengi pamoja na familia zao kuongea na watoto habari za dini yao. Inakadiriwa kuwa

[4] *Reformation and the one World: The Magazine for the theme year 2016* by EKD, page 8.
[5] Number of Protestants Worldwide in Wikipedia
[6] BBC News, 14th of March, 2014, under www.bbc.news
[7] Reformation One World, page 9.
[8] *Ibid*.
[9] Ibid.

kufikia mwaka 2050 idadi ya wakristo na waislamu itakuwa sawa na mwaka 2070 waislamu watazidi wakristo. Hata hivyo, utabiri huu unaweza kubadilika maana nchini china ukristo umeanza kuenea na hivyo kuongeza idadi ya wakristo katika taifa lenye watu wengi duniani (1.3 bilioni).

Pamoja na matengenezo kukazia umuhimu wa Mungu kutenda kila jambo linalohusu kuokolewa kwa mwanadamu, mjadala uliobakia bila jibu ni ule unaouliza kuwa kama kila kitu cha wokovu hufanywa na Mungu tu bila mchango wa mwanadamu. Je, watakaoingia motoni wamlaumu Mungu kwa kuwa hakufanya chochote kuwaokoa? Kwa hakika kumlaumu Mungu kwa ajili ya wale watakaoingia motoni si jambo zuri. Na kama hatuwezi kumlaumu Mungu kwa kutookoa watakaoingia motoni, je tuwalaumu watu wenyewe kwa kutoamini na kumpokea Yesu kama Bwana na mwokozi wao? Na kama tukiwalaumu, je, tunawalaumu kwa ajili ya kitu gani? Matendo fulani? Hapana. Pengine watalaumiwa tu kwa ajili ya kutokubali kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao maana wote waliompokea aliwapa uwezo wa kuwa wana wa Mungu (Yohana 1:24). Ule uamuzi wao wa kukubali au kutokubali kupokea neema utafanya mtu aokoke au la.

Swali hili alipoulizwa mtaalamu wa Matengeneyo ya Kanisa mjini Wittenberg ambaye hutembeza watalii na kuwahutubia mengi kuhusu historia ya Matengenezo ya Kanisa, alisema kuwa matatizo yanayoonekana ndani ya historia ya Matengenezo yamalizwe kwa kusoma neno la Mungu. Alisema kuwa wanamatengenezo walituachia mkazo mzuri wa kupima kila kitu kwa njia ya Neno la Mungu na si kwa kutumia neno la mwanadamu. Kwa njia hii, kuna mambo ambayo tunapaswa kuyaangalia kwa miwani ya Neno la Mungu badala ya kuwalaumu akina Luther kwa maswali ambayo hayajapata majibu ya uhakika kuhusu imani.
Aidha Matengenezo ya Kanisa hayakujihusisha na mambo ya Karama za Roho Mtakatifu maana wanamatengenezo walidhani kuwa mambo ya Karama za Roho Mtakatifu yaliishia kwenye Kanisa la Mwanzo kabla ya kuwepo Vitabu vya Agano Jipya. Hivyo, mkazo wao haukuwekwa kwenye karama hizi japo Neno la Mungu waliloliwekea mkazo lilitaja uwepo wa karama hizi. Miaka 400 baadaye yaliibuka makanisa ya Kipentekoste na kuweka mkazo wa Karama za Roho Mtakatifu ambapo ilianza kuonekana dhahiri kuwa karama za Roho Mtakatifu zipo na zinafanya kazi japo kuna wanaoweka chumvi kwa kulazimisha matokeo ya karama hizo na miujiza.

Miaka miwili iliyopita nilifika kwenye hospitali ya Mkoa kumwona mgonjwa na kumwombea yeye na wenzake. Baadaye alikuja Mchungaji wa Kipentekoste ambaye aliomba vizuri kisha akaanza kuongea kama Yesu. Akawaambia wagonjwa kuwa "wewe utaruhusiwa kesho, wewe pale keshokutwa, wewe pale Jumamosi. Akaongeza kusema kuwa hamuoni yule pale hayupo, nilisema angeondoka leo ameruhusiwa tayari, wagonjwa wakasema ameaga dunia leo asubuhi, Mchungaji akesema basi tumwombee pumziko la amani, akaongea akiwa amenywea kabisa.

Makanisa ya matengenezo kama ilivyo kwa Kanisa la Kirumi yalikazia nafsi ya Mungu Mwana yaani Yesu tu, hayakuweka mkazo kwa Roho Mtakatifu ambaye Marie-Henry Keane anasema kuwa amesahaulika ukilinganisha na Mungu Mwana na Mungu Baba[10]. Mtheologia Mashuhuri Yves Congar anasema kuwa Roho Mtakatifu kwa makanisa ya matengenezo na la Kirumi amebakia kama Mungu afahamikaye kwa

[10] Marie-Henry Keane, "The Spirit of Life" in **Doing Theology**. Ed. John W. de Gruchy, 69.

nusu, wakati Wolfhart Pannenberg anasema kuwa Roho Mtakatifu ameyeyushwa kama maji tofauti na anavyotajwa kikamilifu katika Biblia.

Joseph Ratzinger aliyekuwa Papa wa Kanisa la Kirumi anasema kuwa Roho Mtakatifu amekosa makao katika ulimwengu wa magharibi na Walter Kasper anachangia kuwa Roho Mtakatifu amekosa sura ambapo Johm Macquarrie anaeleza kuwa Roho Mtakatifu kwa makanisa ya matengenezo na Kanisa la Kirumi amekuwa kivuli badala ya kuwa katika uhalisia wake[11].

Hapa tunaona mara moja umuhimu wa kukazia nafsi tatu za Mungu ambaye aliumba (Mungu Baba), akaokoa (Mungu Mwana) na kutakasa, kufariji, kufundisha na kukumbusha yote muhimu katika imani na ufuasi wetu (Roho Mtakatifu). Kwa njia hii Michael Green na Lesslie Newbigin wanasema kuwa kutambua nafsi tatu za Mungu na kuzikazia kwa usawa kutasaidia wafuasi wamwone Mungu katika nyanja zote za maisha: katika uumbaji, katika wokovu na katika hatua za utakaso dhidi ya udunia (secularism) unaomwondoa Mungu katika maisha yote[12].

Ipo haja ya kuangalia matengenezo ya kanisa kwa kuendeleleza mazuri yaliyotokana na Matengenezo haya na wakati huo huo kuona ni mambo gani ambayo hayakuguswa na matengenezo na kuona namna ya kuyatolea maelezo na mafundisho katika kulea na kulinda wakristo walutheri dhidi ya mafundisho potofu yanayoharibu maisha ya watu katika maisha ya sasa na hivyo kuathiri maisha yao ng'ambo ya kaburi.

Katika mada hii, tutaangalia kwa ufupi maisha ya mwanzilishi wa matengenezo, hali ya kanisa kabla ya matengenezo, mafundisho ya msingi ya Dkt. Martin Luther juu ya matengenezo ya Kanisa, matokeo ya matengenezo ya kanisa, kutoelewana miongoni mwa wanamatengenezo, upinzani toka Kanisa la Kirumi, matengenezo kutojali Karama za Roho Mtakatifu na kisha hitimisho.

## 2. MWANZILISHI WA MATENGENEZO NA HALI YA KANISA KABLA YA MATENGENEZO

### 2.1 Maisha ya mwanzilishi wa matengenezo Dkt. Martin Luther

Mwanzilishi wa Matengenezo ya Kanisa si mwingine bali ni Dkt. Martin Luther aliyezaliwa tarehe 10. 11.1483 katika mji mdogo wa Eisleben. Kesho yake ilibidi abatizwe katika kanisa jirani la Mtakatifu Petri Paulo. Ilibidi abatizwe haraka maana watoto wengi nyakati hizo (60%), walikuwa wanakufa mapema kabla ya kufikisha miaka 5 na hivyo familia zilihofia mtoto kufa bila ubatizo jambo ambalo lingewafanya waukose uzima wa milele. Kwa kuwa mtoto alibatizwa tarehe 11 Novemba ambayo ilikuwa siku ya Mtakatifu Martinus, ilibidi mtoto wa mzee Luder aitwe Martinus kwa kilatini yaani Martin.

Baba yake aliyeitwa Hans Luder alikuwa mtoto wa mkulima ambaye aliamua kuhama kwao Thueringia na kwenda Eisleben kutafuta maisha maana kwao asingepata urithi uliokuwa wa mtoto wa mwisho tu. Hata mjini Eisleben maisha hayakwenda vizuri ikabidi ahamie Mansfeld mwaka 1484 ambapo alifanikiwa

[11] Abednego Keshomshahara, "The Lutheran Doctrine of the Holy Spirit and the Challenge of the Spirit Beliefs among the Haya People" (M.Th. Thesis, 2000), 69-88.
[12] Ibid. 81.

kununua kiwanda cha kutengeneza vifaa vya shaba japo alinunua kwa mkopo aliopaswa kuulipa maisha yake yote[13].

Tayari unaweza kuona kuwa maisha ya mwanzilishi wa matengenezo ya kanisa yalikuwa magumu kiasi kwamba Ellen G. White anataja kuwa Dkt. Martin Luther ambaye Mungu alimtumia kufanya mambo makubwa katika historia ya Kanisa, alitokeza katika mazingira ya umaskini kama ombaomba ambapo alipokuwa akienda shuleni wakati mwingine aliimbia watu nyimbo ili apate chakula njiani[14].

Hali hii iliendelea hata alipokuwa mmonaki uliokuwa na maisha ya kuomba msaada kutoka kwa waumini. Tofauti na watoto wenzake, Martin Luther hakufanyishwa kazi nyingi za uchumi wa familia yao japokuwa alilelewa kwa masharti ya hali ya juu kimaadili ambapo wazazi walitazamia utii wa hali ya juu. Hata makosa madogo yalifanya Martin Luther apigwe wakati mwingine kuvuja damu. Baadaye aliona kuwa wazazi walikuwa na nia njema iliyomfanya awe mchapakazi na mwenye nidhamu maisha yake yote[15].

Martin Luther alipelekwa shuleni Mansfeld ambapo alisoma kwa miaka 9 mfululizo bila likizo. Nyakati hizo njia ya kufundisha ilikuwa kuchapa viboko na adhabu kali kiasi kwamba Luther aliona walimu wake kama wakatili na shule kama jehanamu[16]. Walijifunza Kilatini, kusoma, kuandika, na kuimba, na njia mojawapo ya kujifunza ilikuwa kukariri masomo badala ya kufikiri, kuhoji na kuelewa mambo[17]. Baadaye mtoto Martin akiwa na miaka 14 alipelekwa kwenye Shule ya Magdeburg shule ya wanauamsho na kisha baadaye kumtoa na kumpeleka Eisenach kusoma kwene mji mama yake alipozaliwa.

Mjini Eisenach aliishi kwa wakristo matajiri waliomcha Mungu na walikuwa wanadini sana kiasi cha kufanya Martin Luther asikie furaha ya kuishi pale kuliko nyumbani kwao. Matajiri hawa walimtoa Martin alipokuwa anaishi kwa kupanga na kumpeleka kwao kwa kupenda kipaji chake cha kuimba[18]. Familia hii ilifanya Luther apende mji wa Eisenach na pia shule ya pale ilikuwa inaruhusu kufikiri na kuhoji mambo.

Kutokana na jitihada zake katika masomo, baba yake aliamua Martin aende kusoma sheria kwenye Chuo Kikuu cha Erfurt mwaka 1501 akiwa na umri wa miaka 17 ili baadaye aje asaidie wazazi wake wakizeeka[19]. Erfurt ulikuwa mji wa sita kwa ukubwa nchini Ujerumani wakati ule. Katika Chuo Kikuu cha Erfurt, Martin Luther alisoma sheria shahada ya kwanza na ya pili. Akiwa Erfurt ndipo aliona Biblia kwa mara ya kwanza kwenze maktaba za chuo[20]. Mwaka 1502

[13] *Luther, Travel Guide*, English Edition, Published by Schmidt Buch, no date, page 4.
[14] Ellen G. White, *The Great Hope: A revealing Look at the Battle between good and evil- and who wins* (Nairobi: ECDPA), 70-71.
[15] Luther, 4-5
[16] Ibid.5.
[17] Ibid.
[18] Ibdi, 5-6.
[19] James M. Kittelson, *Luther the Reformer: The Story of the Man and his Caree*r ( Minneapolis: Fortress Press, 2003), 50.
[20] Ibid, 6-7.

alihitimu shahada yake ya kwanza ya Sanaa na mwaka 1505 akahitimu shahada ya pili ya Sanaa akawa wa pili kati ya wanafunzi 17 wa darasa lake.[21]

### 2.1.1 Martin Luther kuacha masomo ya sheria ghafla na kuwa Mmonaki/mtahwa.

Martin Luther alianza kusoma sheria 1505. Mwezi mmoja baadaye alitembelea wazazi wake mjini Mansfeld, wakati anarudi njiani ilinyesha mvua kubwa ya radi iliyomtisha kiasi cha kutoa nadhiri akisema: "Mtakatifu Anna, niponye na radi hii, nikipona naahidi kuwa mmonaki au mtawa". Mtakatifu Anna, aliheshimiwa kwa kuwa na wajibu wa kulinda wachimba madini ya shaba na wahunzi wa vifaa vya shaba. Mtakatifu Anna ndiye alikuwa mama wa Bikira Mariamu. Hivyo, pamoja na Baba yake Martin Luther kukasirikia uamuzi wa mtoto wake kuacha masomo ya sheria na kuwa mmonaki, alinyamazishwa na ahadi ya mtoto wake kwa Mt. Anna, mlinzi na msimamizi wa wanaoshughulika na madini ya shaba[22]. Hata hivyo, wazazi wake waliumia kupoteza matumaini ya kutunzwa na mtoto wao uzeeni[23] maana alikuwa ameamua kuingia kwenye huduma isiyoingiza kipato badala yake kutegemea huruma ya wanaochangia wamonaki waweze kuishi[24]. Majibu ya Martin Luther kwa wazazi wake yalikuwa yanashangaza maana aliwajibu wazazi wake kuwa angewasaidia kwa maombi zaidi ya ambavyo angewasaidia akiwa mwanasheria[25].

Baadaye, baba yake Martin Luther alipokea hali ya mwanawe kuwa mmonaki kwa kuwa alikuwa mcha dini. Aliridhia mwanawe awe mmonaki na kumtakia kila la heri katika masomo na maisha. Hans Luder, baba yake Martin Luther alijua kuwa wokovu ni kitu cha kwanza katika maisha.[26] Luther alichagua kuwa mmonaki katika shirika la Mtakatifu Augustine karibu na Chuo Kikuu cha Erfurt badala ya kuwa mbenediktina, mdominikana, au Mfransiskana[27].

Historia inasema kuwa Martin Luther alipofika kwenye nyumba ya wamonaki aliwekwa kwenye kantini kwa miezi miwili kuthibitisha kuwa hakuwa na magonjwa ya kuambukiza yaliyoua watu wengi wakati ule. Wakati wengine walikuwa wanawekwa kantini kwa wiki mbili, yeye aliwekwa kwa miezi miwili, lakini hakukata tamaa. Miezi miwili ilipoisha aliingia umonaki rasmi[28]. Watu wa wakati huo Ujerumani walikuwa hawanywi maji kwa hofu ya magonjwa yatokanayo na maji, badala yake walikunywa pombe kujipoza na kiu. Hata wamonaki walikunywa pombe badala ya maji.

Katika umonaki kazi kubwa ilikuwa ni kutesa mwili ili kuokoa roho. Hatua ya kwanza Martin Luther alinyolewa nywele ili kupata ulinzi wa kichwa ulioonekana kuzidi hata helmeti ya pikipiki. Alijitesa kwa kutokula wala kunywa, alijipiga viboko, kutolala usingizi, kutojifunika wakati wa baridi wala kuvaa koti ambapo miaka kumi baadaye mwili wake ulionekana kama mtu ambaye amejitenga na

[21] Ibidi. 7.
[22] Kittelson, *Luther the Reformer,* 50.
[23] Ibid.
[24] White, *The Great Hope*, 70-71.
[25] Kittelson, *Luther the Reformer*, 50.
[26] Ibid.
[27] Ibid, 51.
[28] Malcolm Walters, Tour guide Expert at Erfurt, 9th of July, 2016.

ulimwengu. Inadhaniwa kuwa hata ugonjwa uliomsumbua baadaye maishani ulitokana na kunyima mwili mahitaji ya msingi.

Alikuwa mtu wa kuomba, kutokula na kujinyima mengi kwa ajili ya kupata wokovu. Ili ampende Mungu kwa moyo wake wote, kwa nguvu zake zote na kwa akili zake zote ilibidi aikatae familia yake, dunia, na yeye mwenyewe kujikana. Baadaye sana Luther alisema kuwa kama angekuwepo Mmonaki wa kwenda mbinguni kwa sababu ya jitihada za kutesa mwili basi angekuwa miongoni mwao[29].

Upande wa kuungama na kutubu dhambi, wamonaki hawakuwa kwenye kundi la wanaotenda maovu ya nje kivitendo bali walikuwa katika kundi la dhambi za hisia, mawazo, nia na kujisikia unakosa kitu fulani kimwili. Hivyo anayeungamisha mmonaki hakumuuliza kutaja dhambi alizotenda kama wakristo wa kawaida bali aliulizwa kama ana mawazo mabaya, nia mbaya, hisia mbaya au kama anajisikia kukosa kitu fulani cha kimwili[30]. Uchunguzi huu wa moyo wa mtu kuhusu hisia, mawazo, nia na mambo unayoyakosa katika maisha kiasi cha kudai toba ya kila saa na kila wakati, kulimfanya Martini Luther amwogope Mungu sana maana alijiona ni mwovu kila wakati na kuogopa hasira ya Mungu na kuona kuwa yeye ni wa kuhukumiwa tu[31].

Luther alichukia maswali ya kuchokonoa siri za ndani ya moyo wa mtu kwa sababu badala ya kumsaidia mtu maswali hayo yalimfanya mtu akate tamaa na kushindwa kuiona neema ya Mungu. Mahali pote ulaya wamonaki waliita majina baadhi ya dhambi kwa namna iliyokatisha tamaa. Kwa mfano kukata tamaa walikuona kama kuwa Chooni, kusononeka kulionekana kama kuwa kwenye uwezekano wa kutenda maovu bila kujali.

Hofu ya Luther ilionekana pale ambapo aliongoza kwa mara ya kwanza Ibada ya Chakula cha Bwana akafikia hatua ya kutetemeka kiasi cha kutaka kuangusha mkate na kikombe cha mvinyo maana alijiona hafai mbele za Mungu. Alisema kwa shida sana maneno yasemayo "huu ni mwili wangu uliotolewa kwa ajili yenu na hii ni damu yangu iliyomwagika kwa ajili yenu"[32].

Ibada hii aliiongoza 1507 mwaka mmoja baada ya kujiunga na umonaki. Baadaye ilikuwepo sherehe kubwa iliyohusisha wazazi wake na ndipo walikutana tangu uamuzi mgumu wa Luther kuacha masomo ya sheria na kuwa mmonaki. Katika sherehe hiyo Luther alimwambia baba yake kuwa haoni ni vizuri mtoto wake kuwa mmonaki na kuongoza ibada ya chakula cha Bwana? Baba yake Luther alimjibu neno ambalo Martin Luther alilikumbuka daima, alimwambia imeandikwa waheshimu baba yako na mama yako, wewe hukuheshimu ushauri wetu wa kwamba usome sheria badala ya kuwa mmonaki.[33]

Mwaka 1510 wamonaki wenzake walimtuma Roma aende kupinga uamuzi wa kuunganisha uongozi wa vituo vya wamonaki maana wapo katika vituo vingine

[29] *Luther the Reformer*, 53-55.
[30] Ibid.
[31] Ibid.
[32] Ibid.
[33] Ibid.

waliokuwa walegevu katika kufuata masharti. Alienda Roma kwa mguu pamoja na mmonaki mwenzake mmoja umbali wa Kilometa 1,100 ambapo kwenda na kurudi ilikuwa Km. 2,200 kama kutoka Bukoba kwenda Morogoro na kurudi kwa miguu. Alipofika Roma alishangaa kupata habari za maovu ya mapdri na kanisa kwa ujumla. Alikuta udunia Roma badala ya utakatifu.[34] Wazo lao la kuzuia umoja wa uongozi wa wamonaki lilikataliwa, wakarudi Ujerumani bila mafanikio.

Baadaye mwaka 1511 Martin Luther alihamia Wittenberg kupisha mivutano na wamonaki wenzake mjini Erfurt ambao walikuwa na mtazamo wa kuwa wamonaki wote ulaya wasiwe na mfumo mmoja wa uongozi. Walipinga mfumo huo maana wao walikuwa wapenzi wa sheria kali za umonaki wakati vipo vituo vingine vya wamonaki havikuwa na sheria kali kama zao.

Luther hakupenda kuendelea na msimamo wa kupinga mfumo mmoja wa uongozi. Aliona afuate mawazo ya viongozi wake, hasa Stauptz aliyeishi Wittenberg, ndipo akahamia Wittenberg kupisha malumbano kati yake na wamonaki wenzake.[35]

### 2.1.2 Luther: Mwanafunzi, Mwalimu wa Theologia, Muhubiri na Kiongozi wa Wamonaki

Luther alihamia Wittenberg mwaka 1511. Baada ya kufika Wittenberg, Staupitz ambaye alikuwa kiongozi wa Wamonaki Wittebnberg alimshauri Martin Luther kuwa ajiandae kuchukua masomo ya Udaktari wa Theologia na awe muhubiri kwenye kanisa la ikulu ya Mfalme. Awali Luther alikataa wito huu lakini kwa kumueshimu kiongozi wake na rafiki yake alikubali kusomea Udaktari wa Theologia na kuwa Muhubiri kwenye Kanisa la Ikulu ya Mfalme.[36]

Tarehe 4.10.1512 Martin Luther alipewa kibali cha kuwa mwanafunzi wa masomo ya udaktari maana alikuwa na sifa, tayari alikuwa na shahada ya pili ya sanaa aliyoipata Chuo Kikuu cha Erfurt kabla ya kuwa mmonaki. Ilikuwa sherehe kubwa ya kupata kibali hicho ampapo aliapa akiwa ameshika Biblia kuwa atatoa mafundisho ya kweli na kutoa taarifa kwa uongozi dhidi ya wapotoshaji wa mafundisho ya kweli.[37]

Baada ya hapo alivishwa kofia maalumu na kupewa pete kama alama ya kibali cha kusomea udaktari wa theolojia. Luther alikuwa na kazi nyingi, kuandika, kujiandaa kusoma na kufundisha, kuhubiri kwenye conventi ya wamonaki, kusoma Neno wakati wa chakula cha wamonaki, kuhubiri usharikani, kuwa Mkurugenzi wa masomo, katika chuo kikuu, kusimamia conventi 11 za wamonaki, kutoa mihadhara juu ya barua za Mtakatifu Paulo, kukusanya mafafanuzi juu ya Zaburi, kusimamia ufugaji wa samaki na kuwa mwamuzi wa michezo.

Martin Luther akaelemewa na kazi kiasi cha kusema kuwa anakosa muda wa kuomba Mungu sala za kila siku na alikosa pia muda wa majaribu ya dunia maana hakujali hata mahitaji ya

[34] *The Great Hope*, 73.
[35] *Luther the Reformer*, 57-63.
[36] Ibid., 83-86.
[37] Ibid., 85.

mwili wake. Alitaja kuwa kwa miezi kadhaa alilalia mashuka ambayo hayakufuliwa kwa jinsi alivyokuwa na kazi nyingi na uchovu mwingi.[38]

Pamoja na kazi nyingi, alipata nafasi ya kuzama zaidi kwenye Neno la Mungu na kupata ufahamu mzuri juu ya haki ya Mungu kati ya miaka ya 1512 hadi 1517 wakati wa matengenezo ya kanisa. Awali alisumbuliwa na mafundisho ya kifalsafa yaliyofundisha kuwa Mungu ni mwenye haki anayeadhibu watu waovu. Kwa tafsiri hii Luther aliona kuwa Mungu ni mbaya anayeadhibu waovu.

Na aliona kuwa kila alipojitahidi kuwa mwema alishindwa na kuendelea kujiona mwovu na asiyestahili mbele za Mungu.[39] Katika kusoma neno la Mungu (Warumi 1: 17) Luther akapata tafsiri nzuri inayoonesha kuwa Mungu mwenye haki huwapa haki wamwaminio kupitia Yesu Kristo. Aliongeza kusema kuwa Adamu wa kale haonekani tu katika matendo maovu tu bali hata kwenye kutenda mema ya kiroho ikiwa ni katika kumwabudu na kumpenda Mungu; maana mwanadamu anapotenda mema ya kiroho anaishia kwenye kujisifu, huku akiwa na nia na malengo yake binafsi. Anajitafutia faida zake mwenyewe na kuyafanya ya kiroho yawe sanamu anayoiabudu.

Hii inatokea kiasi kwamba Mungu anafanywa kuwa sanamu na ukweli wa Mungu hugeuzwa kuwa uongo.[40] Mafafanuzi haya yalikuwa mwanzo wa kuleta matengenezo ya kanisa katika kufahamu kuwa Mwanadamu hawezi kufanya chochote kisheria na kiroho ili aweze kuokolewa isipokuwa ni kwa neema ya Mungu kupitia imani katika Yesu Kristo. Kwamba mwanadamu huokolewa na hivyo mtu asingepaswa kujisifu kwa lolote lile.

Mafundisho haya yalikuwa changamoto kwa mafundisho ya kanisa la wakati huo lililoweka mkazo katika kutimiza mambo mengi ya sheria ili kuokoka. Hapa chini tutaangalia kwa ufupi hali ya kanisa kabla ya matengenezo ya Kanisa ili tupate mazingira kamili yaliyozaa Matengenezo ya mwaka 1517.

### 2.2 Hali ya Kanisa kabla ya Matengenezo ya Kanisa

Volker Leppin na Dorothea Sattler wanasema kuwa kabla ya Matengenezo hali ya kiroho kwa kanisa ilikuwa mbaya. Mapadri na viongozi wa kanisa kwa ngazi zote walikuwa wamepungua uchaji na kushuka kwa maadili yao ya kazi na kwa njia hiyo kukosa ushuhuda wa kikristo hasa kwa wanauamusho wa nyakati hizo.

Maovu mengi yaliyosumbua yalihusu uvunjaji wa amri ya sita kwa kuwa na mahusiano nje ya ndoa.[41] Hali hii ilitokeza upinzani na chuki dhidi ya watumishi wa kanisa. Matokeo yake yalikuwa kuingia kwa walei katika huduma kiasi cha kutokeza ukuhani wa walei waliojituma na hivyo kutokeza “Theolojia ya watu wa Kiroho” badala ya Theolojia ya kitaaluma. Upo umuhimu wa kupima matumizi ya theologia katika makanisa yetu.

Theologia ya vyuoni ni tofauti na theologia ya kwenye maeneo ya kazi. Wakristo wa kawaida hawahitaji kujua mashaka ya waandishi walioandika waraka fulani au aliyeuandika wala kujua mabishano juu ya mwaka wa kuandika waraka fulani. Aidha wakristo hawahitaji kujua jinsi Roho Mtakatifu anavyoitwa kwa Kiyunani (Paraclete). Wanahitaji ujumbe unaogusa maisha yao ya kila siku na kwa hiyo, kama Karl Barth asemavyo: Muhubiri ni vizuri awe na Biblia na magazeti na asikilize redio ili kujua changamoto za jamii na kujibu maswali ya watu akitoa mifano ya maisha ya watu.

[38] Ibid.,
[39] Ibid.
[40] Ibid., 93.
[41] Leppin and Sattler, Reformation, 80.

Kwa sababu hii utashangaa kuona mlei asiye na elimu ya Biblia wala Theologia anachukua wakristo wa mtheologia mwenye shahada moja, mwingine mbili na mwingine ana shahda ya uzamivu. Theolojia ya kiroho ilizama kwenye mabadiliko ya ndani ya mtu kiroho akikutana na Mungu wake badala ya kukutana na Mungu kupitia vitu vya nje kama matendo mema.[42] Uchaji wa moyoni badala ya uchaji wa vitu vya nje vinavyoonekana ndio uliomtawala Luther baada ya kujifunza hali hii kutoka kwa mwalimu wake John Staupitz.

Hapa tunakutana na changamoto ya ushuhuda wetu katika huduma ambapo tunatazamiwa kuishi na kuhudumu kwa uadilifu tukiwa mfano badala ya kuelekeza cha kufanya. Hii ni sawa na hekima ya mfalsafa asemaye kuwa tuwe watu wa kuwa mfano badala ya kutoa mifano. Mfalsafa mwingine anasema kuwa walio wengi hupenda kubadili dunia na watu wake badala ya wao kupenda kubadilika. Hawa ndio husema kuwa fanya nisemayo ila usifanye nitendayo. Tunayosema tunayatenda kiasi gani? Hii nichangamoto kwa ushuhuda wetu.

Uchaji wa kukutana na Mungu kwa mambo ya nje kama vile matendo mema, uliharibiwa na umaskini wa kanisa ambapo Kanisa la Kirumi lilianza kutumia uchaji wa matendo mema kujipatia fedha. Nyakati za Luther yalikuwepo mawazo yaliyokaza kuwa pamoja na uwepo wa neema ya Mungu, mwanadamu angeweza kuokolewa kwa nguvu za kiasili kwa maana ya kuweza kutenda mambo ambayo yangemuokoa dhidi ya kuangamia kiroho.[43]

Hata siku hizi wapo watumishi ambao kwa sababu ya umaskini hukubali kila kitu kinachosemwa na kufanywa na wakristo matajiri bila kuwakemea kwa hofu ya kukosa hela na misaada yao. Kwa njia hii hata taratibu za Kipentekoste huingilia kanisa letu kwa sababu baadhi ya watumishi kukosa msimamo. Ikitokea mtumishi akajikakamua kukataa wazo la tajiri, tajiri akifoka, mtumishi mwingine huogopa na kusema mheshimiwa hutaniwi? Ushuhuda wetu utufikishe kwenye msimamo tunaoukuta kwenye ufunuo kuwa uwe mwaminifu hata kufa nami nitakuvika taji la uzima (Ufunuo 2: 10). Na katika Muhubiri 4: 28 Neno la Mungu linasema pigania ukweli hadi kifo na Mungu atakupigania wewe.

Kanisa la nyakati za kati “medieval age” liliamini kuwa ubatizo uliondoa adhabu ya kurithi toka adamu wa kale ila uovu wa binadamu uliendelea kuwemo katika watu hata baada ya kubatizwa. Hivyo ilionekana kuwa mtu akifa na dhambi ambayo haikuungamwa wala kuitubu, dhambi hiyo ingemfanya abaki kwenye mateso ya moto “purgatory” akiteseka mpaka siku ya kuingia mbinguni. Ili kuepuka mateso ya “purgatory” kabla ya kifo ilibidi mtu asamehewe na kanisa makosa hayo kwa ujumla wake ili mtu asilazimike kugharimia makosa hayo kuzimuni. Ili kusamehewa maovu hayo ilibidi mtu aoneshe ushahidi wa kuwa makini na utayari wa moyo kusamehewa makosa hayo.[44]

Kwa upande mwingine wafu waliokuwa “purgatory” walikuwa hawana uwezo wa kutenda lolote dhidi ya dhambi zao kama kuhiji, kusema sala nyingi za ave Maria, kununua vyeti vya msamaha. Hata hivyo walikuwa na faida ya kwamba wasingeweza kutenda dhambi nyingine kama watu walio hai. Wafu hawa walihitaji pia kufanyiwa msamaha kamili wakifanyiwa utaratibu huo na jamaa zao au rafiki zao kuondoa maovu yaliyofanywa baada ya ubatizo wao bila kujulikana wala kusamehewa. Kutokana na hali hii, kanisa lilifanya utaratibu wa kuuza vyeti vya msamaha ili watu wasamehewe dhambi zilizofanya wateseke kuzimu wakisubiri kwenda mbinguni. Watu waliweza kujinunulia na kununulia jamaa zao waliofariki ili

[42] Ibid.
[43] Ibid.
[44] Ibid., 101.

kujihakikishia au kuhakikisha jamaa zao wanakuwa katika uhusiano mzuri na Mungu bila mateso ya kuzimuni.[45]

Muuza vyeti mashuhuri wakati wa Martin Luther nchini Ujerumani alikuwa Johann Tetzel. Fedha za vyeti vya msamaha zilihitajika kwa ajili ya kujenga upya kanisa la Mt. Peter Basilica mjini Roma. Matangazo ya ujio wake yalitolewa kabla ili watu wamtazamie na kuwa tayari kununua vyeti vya msamaha. Waendesha farasi wengi, wapiga ngoma na tarumpeta walitangaza kufika kwake kila sehemu. Tetzel mwenyewe alisindikizwa na jeshi la Papa Leo X. Katika hotuba yake ya ushawishi kwa watu wanunue vyeti vya msamaha, Tetzel aliwauliza watu: "Je hamsikii sauti za jamaa zeu waliofariki na wengine wakilia na kusema tusaidie, tuhurumie maana tunaungua motoni na mnaweza kutuokoa kwa kutuombea msamaha? Na hamtaki?" Tetzel aliendelea kusema "Hela inapodondoka kwenye sanduku la hela, roho ya mtu huenda mbinguni mara moja."[46]

Kabla ya ujio wa Tetzel mjini Wittenberg, kulikuwepo watu wengi waliotilia mashaka utaratibu wa vyeti vya misamaha kwa maana ya kwamba baadhi ya watu wa ulaya waliona mfumo huu kama unyonyaji wa Italia kunyonya maeneo mengine ya ulaya. Maana yake kabla ya upinzani mzito toka kwa Luther, tayari Tetzel alikuwa akikutana na upinzania mdogo mdogo dhidi ya sera yake ya kukusanya mapato ya kupeleka Roma.[47] Kama tutakavyoona baadaye, uuzaji wa vyeti vya msamaha ndio ulilipua upinzani mkubwa dhidi ya Kanisa la Kirumi na hivyo kuwa chanzo kikubwa cha Matengenezo ya Kanisa.

## 3. DKT. MARTIN LUTHER KUANZISHA MATENGENEZO YA KANISA 1517

### 3.1 Utangulizi

Wakati Johann Tetzel alipokaribia Wittenberg, mkesha wa kuamkia siku ya Watakatifu 1517, Profesa kijana wa Theolojia Dkt. Martin Luther alibandika hoja 95 dhidi ya uuzaji wa vyeti vya msamaha. Hoja hizi ziliandikwa kwa lugha ya Kilatini kwa ajili ya wasomi wa wakati ule. Aidha, hoja hizi zilitafsiriwa mara moja katika lugha ya Kijerumani kwa ajili ya kusaidia watu wa kawaida. Watu wakaanza kusambaza vikatuni vinavyoonesha kuwa upendo na neema ya Kristo vinazidi vyeti vya misamaha katika kutoa wokovu. Luther kama Mchungaji alipenda kutunza roho za watu dhidi ya mafundisho mabaya yaliyowatesa kinafsi na kiuchumi. Aidha, kama mwalimu wa Chuo Kikuu alikuwa ameapa kusema ukweli na kukemea uongo.[48]

Wakati Luther anatundika hoja 95 hakuwa amefikiria mapinduzi makubwa ndani ya kanisa bali alipenda kulisaidia kanisa liache mambo mabaya ya kuuza vyeti vya msamaha. Aliona kuwa ndani ya mfumo wa awali, kuuza vyeti vya msamaha kunaondoa watu kwenye toba ya kweli na matendo mema ya kweli. Na kuwa matendo kama haya yanafanya wasomi washindwe kutetea heshima ya kanisa. Luther alisema baadaye kuwa kama jambo hili lingerekebishwa bila hasira pengine kutengena kusingekuwepo.

Kanisa la Kirumi lilimpa Johann Tetzel udaktari wa heshima ili ajibizane na Luther wakiwa na kiwango sawa cha elimu. Luther alishauri kanisa kuwa ni vizuri watu wachangie ujenzi wa Kanisa moja kwa moja bila kupitia njia ya vyeti vya msamaha. Maana mchango wa kujenga kanisa ni kwa ajili ya Mungu wakati mchango wa vyeti vya msamaha ni kwa ajili watu si kwa ajili ya Mungu.

Luther alikazia kuwa dhambi ni kutomwamini Kristo. Ukristo ni safari ambayo haijaisha, ukristo ni mapambano, siyo ushindi, siyo ya kuwa na haki bali ya kufanywa wenye haki, siyo

[45] Ibid., 101-103.
[46] Ibid., 103-104.
[47] Ibid. 104.
[48] Ibid., 106-108.

ya kuwa na utakatifu bali hatua za kufanywa watakatifu mara kwa mara. Na kuwa si rahisi kupata utakatifu katika maisha haya. Luther akaona kuwa kwa njia ya imani katika Yesu Kristo tunakuwa huru dhidi ya sheria ambayo ni vizuri iwepo bila kuogopwa. Na tunakuwa huru dhidi ya kifo ambacho kipo lakini hatupashwi kukiogopa.[49]

### 3.2 Matengenezo kama Vuguvugu la Uhuru wa Mkristo.

Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa Matengenezo yalibeba ujumbe wa uhuru wa binadamu, uhuru wa Mkristo mbele za Mungu, uhuru mtakatifu wa watoto wa Mungu. Matengenezo yalionesha imani kama mwanzo wa hatua ya kuelekea uhuru na waokovu. Na hapo Luther alimfahamu Mungu kama Mungu wa uhuru, na kuwa mwanadamu hawezi kujiokoa mwenyewe isipokuwa anaokolewa kwa neema kwa njia ya imani katika Yesu Kristo.[50] Luther alipinga mamlaka ya Papa na Kanisa hasa juu ya mikazo ya matendo ya sheria katika wokovu wa mwanadamu. Kutokana na msimamo wake, Papa alikataza mafundisho ya Luther na kuagiza auawe baada ya Luther kukataa kukana mafundisho yake.

Aidha Kanisa la Kirumi liliagiza vitabu vya Luther vichomwe na kuteketezwa. Luther naye alichoma hadharani barua ya Papa kwa ulimwengu. Luther aliona kanisa la Kirumi wakati ule likiwa kwenye utumwa Babeli kama vile taifa la Israeli lilivyokuwa utumwani, na alimwona Papa kama Mpinga Kristo. Papa na kanisa lake walifikia hatua ya kumuona Luther kama shetani ndani ya sura ya binadamu na vazi la umonaki.[51] Naye Luther aliona Roma ilikuwa mbaya kuliko Uturuki.[52] Kanisa la Kirumi lilifanya kila jitihada ili Luther abadili msimamo wake lakini Luther hakukubali na akafikia kusema kuwa “Sibadili msimamo wangu, mpaka nithibitishiwe makosa yangu kwa njia ya Neno la Mungu, hapa nasimama, Mungu nisaidie”.

Luther aliogopa sana kwenda Roma alipoitwa maana karne moja kabla ya hapo mtu aitwaye Jan Hus aliuawa mbele ya Halimashauri ya Kanisa la Kirumi kwa kosa la uzushi.[53] Ni wakati huu alipotunga wimbo wa 302 katika TMW: “Mungu wetu ndiye Boma silaha tena ngao, atukingiaye shida zitushikazo sisi, adui wa kale afanya hila ya kutushinda, ni mwenye nguvu kuu, hakuna amwezaaye.”

Hoja zake zilionesha mkristo kama mtu huru juu ya yote na asiye chini ya yeyote. Wakati huo huo mkristo ni mtumishi wa wote na mtumwa wa kila mtu. Ni kwa mtindo huu alieleza kuwa mkristo ni mtakatifu na mwenye dhambi maana anakiri udhaifu wake anapokiri na kutubu dhambi na wakati huo huo anatangaziwa msamaha na hivyo ni mtakatifu mwenye dhambi. Kuongea sentensi zinazopingana ilikuwa njia ya kuongea nyakati hizo.

Martin Luther alitumia mawazo ya mfalsafa Plato aliyetumiwa pia na Mtume Paulo katika kuona kuwa mwanadamu anaishi katika mivutano ya mwili na roho ambapo Mkristo anaishi kwenye mivutano ya kimwili na kiroho. Hali hii inaelezwa kwa njia ya Adamu wa kale na mtu mpya, na kwa hiyo mtu kujikuta anaishi katika sehemu mbili tofauti kiasi cha Paulo kusema kuwa analotaka kufanya silo afanyalo, hujikurta anafanya asichopenda. Yesu naye anaongea kwa lugha hii ya kuwa roho iradhi lakini mwili ni dhaifu.[54] Mtume Paulo anadhihirisha mvutano huu katika Wagalatia 5:16 anaposema: “Basi enendeni katika Roho wala hamtatimiza kamwe tamaa za mwili, maana mwili hupingana na Roho na Roho hupingana na mwili kiasi kwamba hamuwezi kutenda mpendalo, lakini mkiwa katika Roho hamko tena chini ya sheria.”

[49] Ibid., 106-109.
[50] Lecture Notes, Reformation Theology, Kirchliche Hochschule Wuppertal/Bethel, Bethel.
[51] *The Great Hope*, 98.
[52] *Luther the Reformer*, 135.
[53] Ibid, 118-119.
[54] Lecture Notes.

Kwa mtazamo huu, Luther aliona kuwa mwili kama mambo ya nje, hauwezi kuhusika kwenye kukomboa roho ya mtu na wala hauhusiki katika wokovu wa mtu. Kwa njia hii matendo mema hayamfanyi mtu kuwa mwema bali mtu mwema hutenda matendo mema. Kinachookoa roho ya mtu ni Neno la Mungu linapohubiriwa, maana yake roho haiwezi kujiambia Neno la Mungu ni mpaka iambiwe ndipo iwe huru.[55] Kwa msingi huu, theologia ya Luther ikawa theologia ya Neno yaani Neno lenye nguvu ya neema katika kumfanya mtu awe huru. Ujumbe huu haukupendwa na watu waliokuwa wamezama katika matendo ya kisheria.

### 3.2.1 Kuokolewa kwa Mwanadamu na Uhuru wa Mwanadamu

#### 3.2.1.1 Imani tu, Neema tu, Neno la Mungu tu, na Kristo tu

Katika mafundisho ya matengenezo, Luther aliweka mkazo juu ya imani peke yake katika kumwokoa mwanadamu bila matendo ya sheria. Kwa Luther sheria ilibaki kusaidia kuleta utulivu katika jamii na kisiasa. Aidha sheria ilionesha mtu dhambi zake bila kumwokoa na hivyo kumfanya awe mhitaji wa toba na neema ya Mungu. Haya yote yanawezekana kwa njia ya kumwamini Yesu Kristo ambaye anahubiriwa kupitia Neno la Mungu liokoalo. Kwa hiyo ujumbe wa matengenezo ulileta uhuru kwa wakristo dhidi ya mzigo wa sheria ambazo ilikuwa vigumu kuzitimiza. Luther alikaza kuwa uwezo wa mtu kuamua ulibaki katika mambo ya nje na si mambo ya ndani au ya kiroho. Hapa alikuwa kinyume na akina Pelagius waliosisitiza kuwa mwanadamu anao uhuru wa kukataa au kukubali neema hata baada ya anguko kuwepo.

#### 3.2.1.2 Tatizo la Uhusiano wa Kanisa na Serikali, Mambo ya kiroho na mwili

Tatizo lililojitokeza lilikuwa jinsi ya kuhusianisha kanisa na serikali, mambo ya kiroho na ya kimwili. Wakati huu Luther alikuwa amepinga kanisa kujihusisha na mambo ya utawala wa falme na mambo ya siasa kufikia hatua ya kusahau wajibu wa msingi wa kanisa. Luther aliona kuwa zipo falme mbili za Mungu, ufalme wa kiroho (kanisa) na ufalme wa kutawala dunia. Ufalme wa kanisa ulionekana kutawala kupitia Yesu Kristo kwa kutumia Injili iokoayo. Na ufalme wa dunia unatawala kupitia Mungu Baba kwa njia ya sheria na hivyo hutumia nguvu na upanga. Luther aliona kuwa Injili katika ufalme wa kanisa inakamilisha sheria ya ufalme wa dunia.

Aidha, Luther aliona kuwa kanisa liheshimu serikali kwa mambo ya nje au ya kimwili na serikali iheshimu kanisa kwa mambo ya kiroho. Luther alifundisha kuwa kanisa halikuwa na mamlaka ya kulazimisha yeyote isipokuwa lilipaswa kukemea maovu na kuhubiri mapenzi ya Mungu hata kama msimamo huu ungesababisha vifo vya waumini.[56] Klaus Nürnberger anathibitisha kuwa kwa sababu ya machafuko ndani ya kanisa, Luther alivunja kanuni ya kutenga kanisa na serikali pale alipoona ni vizuri wafalme waongoze kanisa ili kuleta amani na utulivu. Hata makubaliano ya amani kati ya wakatoliki na waprotestanti ya mwaka 1555 yalitoa mamlaka kwa wafalme kuamua dini ya raia wao ambapo iliamriwa kuwa kila raia afuate dini ya mfalme wake ili kuondoa migongano na vita (Cuius regio eius regio), uamuzi ulioleta madhara makubwa baadye[57] hasa baada ya watu kuingia katika falme mbalimbali wakiwa na dini tofauti na ile ya mfalme na watu wake.

**Mkazo** wa Luther umechangia matatizo ya jinsi ya kuhusika kwa kanisa katika mambo ya kijamii na kisiasa baada ya kutenga kiasi fulani mambo ya kiroho na mambo ya kisiasa. Kwa mfano, kanisa la Ujerumani halikujihusisha na kupinga maovu ya utawala wa Hitler hadi hapo

---

[55] Ibid.

[56] Klaus Nürnberger, **Martin Luther's Message for us Today: A Perspective from the South** (Piertermaritzburg: Cluster Publications, 2005), 257ff.

[57] Ibid., 258.

Dietrich Bonhieffer alipokemea kanisa na kusema kuwa halipashwi kunyamazia uovu wa Hitler. Baadaye Bonhoefer alifikia hatua ya kupanga kumuua Hitler ili kuzuia uovu uliokithiri. Alitambua kuwa kuua ni jambo baya ila aliona kuwa alikuwa anazuia mauaji makubwa yaliyokithiri na kwa hiyo aliona ni vema avunje sheria ili aokoe sheria, aue ili kuzuia mauaji ya halaiki.

Luther alifikia hatua ya kusema kuwa mtu binafsi anapovamiwa aamue kutumia kanuni ya hotuba ya mlimani ambapo ukipigwa umgeuzie shavu la pili adui yake na iwapo serikali au ufalme ungevamia basi mkristo awe tayari kulinda na kutetea nchi yake. Hapa Luther anaweka kanuni mbili, moja ya kutolipiza kisasi ukiwa binafsi na ukiwa katika jamii mkavamiwa, basi uwe tayari kulinda na kupigania taifa lako. Kuhusu hotuba ya mlimani inayodai tusijitetee tunapoumizwa, Thomas Acquinas anasema kuwa mwongozo huu ni kwa ajili ya wakristo wachache wasio wa kawaida kama Wachungaji lakini waliobakia watumie sheria ya asili inayoruhusu kujitetea na kulipiza visasi.

Msimamo wa kutenga wachungaji na walei katika ufuasi uliondolewa na Matengenezo ambayo yaliona kuwa watu wote ni sawa mbele ya Mungu, hakuna wa kawaida na asiye wa kawaida. Kwa Mtakatifu Augustino hotuba ya mlimani ni kipimo cha mfuasi wa kweli na ni uhakikisho wa amani na uwepo wa ufalme wa Mungu. Tatizo ni pale ambapo jamii haina wakristo tu wa kufuata kanuni hii kiasi kwamba wasiofuata kanuni hii watatesa wakristo kila wakati maana hawako tayari kujitetea.[58]

Mwanamatengenezo Kalvin yeye hakupenda mtazamo wa Luther wa kutenga eneo la kutawaliwa na kanisa na eneo la kutawaliwa na dunia bali alisisitiza kuwa Kristo ndiye mtawala katika falme zote mbili, duniani na kanisani ili ushawishi wake uwe sehemu zote, kanisani na duniani japo mtazamo huu ungeleta shida shehemu zenye dini tofauti.

#### 3.2.1.3 Ukuhani wa waumini wote

Mkazo huu ulileta mabadiriko yaliyofanya kila mkristo awe huru kuhusiana na Mungu wake bila kuwa na mtu mwingine katikati wa kumuhusianisha na Mungu. Watu wangeweza kuomba Mungu moja kwa moja bila kuhani. Haya yalikuwa mafundisho yaliyoleta uhuru kwa wakristo na kuondoa utegemezi wa kiroho kwa makuhani au mapadri. Tatizo lililojitokeza ni kuondoa mfumo wa uongozi wa kanisa ambapo karibu kila mtu alijiona anaweza kujiongoza bila mfumo wa uongozi wa kanisa.

Hata hivyo, ilitokea changamoto ya hitaji la uongozi wa kanisa maana kanisa lisingekuwepo bila uongozi rasmi. Ndipo ilionekana kuwa lipo hitaji la Mchungaji wa kupewa ofisi ya kutumika kutoa huduma ya Neno na Sakramenti. Baadaye lilikuwepo hitaji la mfumo wa kuunganisha Wachungaji wote chini ya uongozi mmoja ndani ya ufalme au eneo husika. Kwa njia hii uongozi wa wanamatengenezo haukuwa na mfumo wa utawala wa dunia nzima. Ni hivi karibuni ambapo Makanisa huru ya yameunda mashirikisho ya kuwaunganisha kimataifa kama vile Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani na Umoja wa Makanisa ya Kiprotestanti duniania.[59]

---

[58] Abednego Keshomshahara, "Peace as a Central Task of the Christian" in **Reconciliation and Just Peace** (Wien: Lit Verlag, 2016),144-147

[59] Volker Leppin and Dorothea Sattler Eds. **Reformation, 1517-2017: Ökumenische Perspektiven** (Herder, 2014), 105ff.

### 3.3 Upinzani dhidi ya Dkt. Martin Luther miongoni mwa wanamatengenezo

#### 3.3.1 Mpinzani wa Luther: Thomaz Muenzer na mkazo wa Uhuru wa kiroho kuleta uhuru wa kisiasa na kiuchumi

Thomas Munzer, mtheologia aliyesomea Leipzig alikutana na Luther mwaka 1520, alikuwa na itikadi kali ya kuhakikisha uhuru wa kiroho unagusa maisha ya kiuchumi na kisiasa na hivyo kupanua wigo wa uhuru wa Mkristo katika nyanja zote za maisha. Wakati huo walikuwepo wakulima waliokuwa wakinyonywa na wamiliki wa mashamba. Kitendo cha kutokea kwa matengenezo ya kanisa kilitafsiriwa kama uhuru katika nyanja zote za maisha, kiroho na kiuchumi. Mtetezi wa wakulima alikuwa Thomas Munzer aliyechukia kuona Luther anazuia matengenezo ya kanisa yasitumiwe na wakulima kupigania haki zao dhidi ya wafalme.

Munzer alimlaumu Luther kwa kuweka breki kwenye matengenezo na kufanya matengenezo yawe ya kiroho tu bila kupigania wakulima. Munzer alifikia hatua ya kumuita Luther kuwa ni Dokta Mwongo (Doktor Luegner) na kumwona papa katika sura mpya kwa kuwa hakupanua ukombozi wa kiroho uguse maisha yote.[60]

Thomas Muenzer alipenda utawala wa dunia uondolewe ili Kristo atawale mifumo yote ya maisha ikibidi kwa kutumia nguvu, jambo alilolikataa Luther kwa kukazia falme mbili za utawala wa mwandadamu, utawala wa kiroho na utawala wa kidunia. Wakati huo Luther alimlaumu Thomas Muenzer kwa kutokuwa mvumilivu na kuwa mleta fujo katika jamii katika miwani ya dini. Walikuwepo wanauamsho wa kinabii waliomfanya Munzer awe na itikadi kali. Aliongoza maandamano ya wakulima dhidi ya wafalme. Wafalme walitumia nguvu kuteketeza maandamano na kumkamata Thomas Muenzer wakamtesa na kumyonga mwaka 1925.

Mfalsafa Ernest Bloch aliyependelea sana kuhusika kwa imani na matumaini katika kuletea dunia maendeleo anamsifu sana Thomas Muentzer kwa kuweka imani katika maisha na kuleta ukombozi. Ernest Bloch anasema kuwa kanisa lisiwe na picha ya Yesu aliye mwana kondoo likanyamazia ukandamizaji bali pia liwe na picha ya Yesu aliye simba wa Yuda, mkali dhidi ya unyonyaji wa kila aina. Kwake Bloch, Yesu alikuwa mwanadamu aliyekufuru kujiita Mungu lakini kwa lengo la kuwatoa watu kwenye mawazo ya mbinguni na kuwaleta duniani, aliwatoa watu kwenye mawazo ya kufikiri Mungu ndiye atafanya kila kitu na mwanadamu awe mtendewa tu. Bloch anasema kuwa Yesu kama mwanadamu alijiita Mungu akionesha kuwa Mungu anatenda kazi ndani ya wanadamu na hivyo kuujenga ufalme wa Mungu bila Mungu. Mtheolojia Jürgen Moltmann anaona kuwa imani inayowekwa katika miasha ikatetea watu na kuwakomboa ndilo tumaini linalopambana badala ya tumaini tendewa lisilojishughulisha na chochote likisubiri tu faraja ya mbinguni.

Luther aliona tatizo la wakulima lakini hakupenda Injili itumike kupigania mambo ya kimwili. Alishauri watumie sheria za serikali kupigania haki zao ila serikali ikatumia nguvu kuwakandamiza wakulima. Tayari mafundisho ya kutenga falme mbili za Mungu, ufalme wa dunia na ufalme wa kanisa kulileta shida ya kuhusianisha mkristo na serikali[61].

#### 3.3.2 Waliotetea uwezo wa Binadamu katika kuamua mambo ya kiroho

Vuguvugu hili liliongozwa na Desiderius Erasmusu wa Rotterdam. Yeye alitetea msimamo kuwa hata baada ya anguko, mwanadamu alibakiza kiasi fulani uhuru wa kuamua kutenda mema ya kiroho na ya kidunia. Walikazia kuwa huwezi kujiokoa lakini unao uwezekanao wa kufungua moyo wako au kuufunga dhidi ya wokovu. Mtazamo huu ulikuwa tofauti na ule wa

[60] Lecture notes, KIHO, 2005.

[61] **Kirche im Wandel der Zeit**, 18-19.

Luther ambaye alikaza kuwa mwanadamu hawezi kuamua lolote kuhusu wokovu wake maana kila kitu kuhusu wokovu ni kazi ya Mungu, mwanadamu anaweza kuamua tu ya kimwili lakini ya kiroho hana uamuzi wowote.

Mkazo wa uwezo wa binadamu ulikuwa mkazo wa waliotetetea Utu na heshima ya mwanadamu (Humanismus) dhidi ya ujinga, ufisadi na unyonyaji. Mwanzoni Luther na watu wa Utu walihusiana vizuri ila baadaye walitengwa na jambo la uhuru wa mtu kuamua mambo ya kiroho, jambo alilolipinga Luther. Aidha, watu wa utu waliona kuwa Luther alitumia lugha ya juu isivyo lazima kwa watu wa kawaida na kuwa Luther alikuwa hapokei mawazo ya wengine.

Kwa Erasmus, kwa njia ya elimu mtu hujifunza mengi na hivyo kushughulikia ukweli na kupambana na uovu na unapofika mwishoni ujue kuwa ni neema ya Mungu imekuwezesha hata kama nia yako imehusika mwanzoni. Kwake Erasmus, mambo ya kwenye Biblia mengine huhitaji elimu, hakukazia mambo ya ‘dogma’ bali kuongozwa na mahitaji ya kimaisha. Kwa Erasmus, kama mtu hana uwezo wa kufanya jema kiroho, basi pasingekuwepo dhana ya adhabu wala ya zawadi kwa watakaoishi na kutenda vema. Erasmus aliongeza kusema kuwa ni kweli ilikuwepo sababu ya kupinga walioweka chumvi katika matendo ya kulipa fedha za vyeti vya misamaha na kulipia fedha wafu ili watoke motoni ila aliongeza kusema kuwa Luther naye aliweka chumvi kwa kutotambua matendo ya watakatifu na uhuru wa kuamua kupokea neema au kuikataa.[62]

Kuhusu kuhusika kwa Mungu katika mambo yote ya kuokolewa kwa mtu yalileta maswali kuhusu nguvu za Mungu katika kushinda maovu na uovu ambapo ilihojiwa kwa nini Mungu anaacha maovu na shida ziwepo. Katika kuonesha uwezo wa Mungu Luther alisema kuwa Mungu ndiye huongoza kila kitu maana Mungu ni yote katika yote. Aidha, Mungu ndiye alimuumba shetani ambaye huleta matatizo japo Mungu hutenda kazi yake kwa njia ya wabaya. Na kuwa shetani hawezi kutenda lolote bila Mungu kwa kuzingatia mfano wa jinsi Mungu alivyofanya moyo wa Farao uwe mgumu. Hata hivyo Luther alitambua mipaka ya fahamu zetu na kusema kuwa katika umilele tutaweza kutambua haki ya Mungu kwa wanaookolewa na wasiookolewa.

Shida ya haki ya Mungu na changamoto ya matatizo ya wanadamu iliendelea kuleta maswali hadi karne ya 17 ambapo William Leibnis alitokeza kanuni 3 za milele juu ya vyanzo vya matatiyo ya binadamu duniani:

(i) Mungu kutoweza kuumba Mungu mwingine na hivyo kila kilichoumbwa na Mungu kina udhaifu.
(ii) Mungu kuweka sheria za asili zitawale bila yeye kuingilia na kuweka mianya michache ya muujiza
(iii) Mungu kumpa uhuru mwanadamu aamue kutenda jema au baya bila kumlazimisha atende jema.

### 3.3.3 Upinzani kutoka kwa Zwingli

Zwingli alikuwa mwanamatengenezo kutokea Uswizi eneo linalozungumza Kijerumani. Zwingli alitoa changamoto kwa Luther alipokazia kuwa Mungu hayuko katika sehemu 2 za Mungu aliyejificha kisheria (Deus Abskonditus) na Mungu wa Neema aliyejifunua katika Yesu Kristo (Deus Revelatus) maana Mungu ni yote katika yote. Zwingli alisema kuwa hatupashwi kumtenga Mungu katika sheria na Injili. Zwingli alifundisha kuwa sheria ni nzuri maana hutueleza mapenzi ya Mungu na kuwa sheria na Injili vyote tuvihubiri. Kwa Zwingli,

[62] Lecture notes, Kirchliche Hochschule, Bethel.

anguko la Mwanadamu lilisaidia mtu kufahamu haki ya Mungu na mpango wake wa kumtuma Yesu aje duniani kutuokoa. Wema wa Mungu ukaonekana ndani ya anguko la mwanadamu.

Upinzani mkubwa wa Zwingli dhidi ya Luther ulihusu Chakula cha Bwana ambapo Luther na Jean Kalvin walikazia kuwa Bwana Yesu yumo kwenye mkate na mvinyo kwa njia ya imani na neno,[63] maana Yesu alisema huu ni mwili wangu na hii ni damu yangu imwagikayo kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Kwa Zwingli Yesu hakuwemo kwenye mkate na mvinyo bali ilikuwa ni ukumbusho wa tukio la kufa kwa Yesu,[64] fanyeni kwa ukumbusho wangu, kwani Yesu hawezi kuwemo kwenye mkate na mvinyo wakati tayari alishapaa mbinguni ameketi mkono wa kuume wa Mungu baba Mwenyezi. Zwingli na wafuasi wake waliona kuwa Luther amekuwa karibu sana na Wakatoliki ambao katika ibada ya Chakula cha Bwana huamini kuwa mkate na mvinyo hubadilika viasili vyake kabisa kabisa na kuwa mwili na damu ya Yesu.

### 3.3.4 Upinzani toka kwa Jean Calvin

Jean Calvin alikuwa mwanamatengenezo toka kwenye eneo lililozungumza kifaransa. Wakati Luther alikazia mpango wa Mungu kuteua mapema watu wote waokolewe, Calvin aliona kuwa Mungu alishaamua mapema watakaookolewa na watakaoteswa milele jehanamu. Mkazo wa Kalvin juu ya Mungu kupanga mapema watakaookoka na watakaoangamia yalifanya wafuasi wake baadaye wajihoji namna ya kujua walioteuliwa na Mungu. Jibu la wafuasi wa Kalvin likawa ni kwamba atakayekuwa na maisha mazuri ya ufanisi hiyo ni alama ya kuwa ameteuliwa. Matokeo yake wafuasi wa Kalvin wakaanza kulimbikiza mali na fedha kama njia ya kutambua na kuhakikisha kuwa wameteuliwa.

Aidha, walibana matumizi katika kutunza mali na kukazia kuwa watu wema, kufanya kazi kwa bidii na kutoa sadaka ili usipoteze uteule. Walijizuia mambo ya raha kama kwenda kwenye dansi, wakawekeza ili kupata zaidi na matokeo yake wakawa mapepari. Uhusiano wa mafundisho ya Calvin na upepari uligunduliwa na Max Weber katika kitabu chake cha “Protestant Ethics and the Spirit of Capitalism”. Kwa Calvin, Mungu anapanga apendavyo kwa utukufu wake, wengine amepanga waokoke na wengine waangamie, kwa Mungu hata tunaloona ni baya linaleta utukufu kwake.

### 3.3.5 Wapinzani wa kujenga ufalme wa Kristo duniani

Mjini Muenster kulitokea waliotaka kujenga ufalme wa Mungu duniani. Pamoja na Luther kuwaonya mara kadhaa mwaka 1932 wakatokea wakibatiza watu upya mijini. Walitaka ufalme mpya wenye haki na walifikia hatua ya kuondoa maadhimisho ya Jumapili, waliishi kwa ujamaa, wakiwa na ndoa za wake wengi, walichoma vitabu isipokuwa Biblia. Mwaka 1935 kundi hili lilishambuliwa na kufanya matengenezo katika eneo hilo yakwame na usharika wa kimatengenezo ukafikia mwisho.

### 3.3.4 Waliokataa ubatizo wa watoto wadogo

Hawa walikataa ubatizo wa watoto na kuamua kubatiza watu wazima walioamini. Waliishi kwa Neno na maombi. Kwa kuwa walikataa ubatizo wa watoto, walionekana mbele za serikali kama maadui. Walifatiliwa na kufungwa na wengine waliuawa kwa kunyongwa na kuchomwa moto. Luther aliona ni vema walindwe ila wakataliwe mafundisho yao bila matumizi ya nguvu. Hata hivyo walishambuliwa wakakimbilia maeneo mengi ya ulaya. Wafuasi wa mtazamo huu ndio walitokeza makanisa ya kimenonaiti na wabaptisti.[65]

[63] Kirche im Wandl der Zeit: Reformation bis Gegenwart (Wuppertal : R. Brockhous Verlag, 42)
[64] Ibid, 22.
[65] *Kirche im Wandel der Zeit*, 20-21.

## 4. Matengenezo na Karama za Roho Mtakatifu

### 4.1 Matengenezo kutojali Karama za Roho Mtakatifu

Matengenezo ya Kanisa hayakujali mambo yahusuyo karama za roho mtakatifu. Wanamatengenezo walijihusisha sana na kazi ya msingi ya Roho Mtakatifu kama vile Neno, ushuhuda, kuhesabiwa haki bure, utakaso, na wokovu kwa ujumla. Kazi za Roho Mtakatifu kwa upande wa Karama zake katika kujenga wakristo na kutimiza mahitaji yao ya muda mfupi mfupi, ni jambo ambalo wanamatengenezo hawakulipatia mkazo. J. R. Williams anaona kuwa wakati umefika kujifunza mengi kuhusu karama za Roho Mtakatifu ili kuweza kukabiliana na changamoto za wakati wetu maana Karama za Roho Mtakatifu ni wimbi kubwa lenye nguvu katika makanisa ya kiprotestanti kama lile la wakati wa matengenezo ya kanisa karne tano zilizopita.[66]

Barker anaongeza kusema kuwa ni vizuri kuhusianisha mafundisho ya matengenezo na wimbi jipya la Karama za Roho Mtakatifu ili kujenga msingi mzuri wa imani bila kuacha pande mbili hizi zikiwa tofauti[67] au kupingana na kupotosha watu.

Wanamatengenezo waliona kuwa karama za Roho Mtakatifu ziliishia kwenye kanisa la mwanzo baada ya kifo cha mtume wa mwisho na baada ya Biblia kuandikwa na kuwekwa pamoja.[68] Hata hivyo makanisa yanayokazia karama za roho mtakatifu huona kuwa karama za Roho kama zinavyotajwa katika 1Wakorintho Sura ya 12 kama vile kunena kwa lugha, uponyaji wa miujiza, kuondoa pepo wachafu, na unabii ni karama ambazo zipo na zinajenga kanisa.[69] Matokeo yake ni kuwa na wakristo katika makanisa ya kihistoria wanaokubali kuwa karama hizi zipo kanisani hata siku hizi na wapo wengine hutilia mashaka karama hizi kama zipo kweli.[70]

### 4.2 Changamoto za Karama za Roho Mtakatifu siku hizi

Changamoto za karama za Roho mtakakatifu ni nyingi hasa kwa kuona kuwa baadhai ya wakristo wenzetu wamehamia madhehebu ya kipentekoste na wengine wamebaki katika makanisa ya matengenezo. Baadhi ya walutheri wanahudhuria mafundisho ya kipentekoste wakati wanaishi katika makanisa ya kilutheri. Wengine husali asubuhi katika kanisa la kilutheri na jioni kwenda makanisa ya kipentekoste. Wengine waliohamia makanisa ya kipentekoste wamelazimika kurudi baada ya kujeruhiwa na mafundisho ambayo huwaletea matatizo kama vile kuwazuia kwenda hospitalini kwa kukazia maombi tu na wengine kuwazuia kutumia dawa za mitishamba wakati Hezekiel 47:12 neno linasema Mungu ameweka mimea na mitishamba tukaitumie kama dawa. Lililobaya ni kutumia dawa ya mitishamba kwa masharti ya kishirikina kama kutumia dawa ukiwa uchi na kuzunguka nyumba mara kadhaa.

Nchini Namibia kuna wanaorudi kwenye kanisa la Kilutheri ili wazikwe kilutheri kwenye makanisa yao ya awali. Lengo la kurudi kuzikwa inabidi lifanyiwe utafiti (Askofu wa Namibia, Juni, 2016, Ujerumani).

Wengine wanazuia watoto wao kusoma kwa kuwaambia kuwa ushindi wataupata kwa miujiza tu. Watoto wanatumia muda mwingi kuomba na kufunga bila muda wa kujisomea. Wengine wameingia katika uaguzi wa kutambua wachawi na kusabanisha maafa kijamii ambapo

---

[66] Read Paul Elbert, *"Calvin and the Spiritual Gifts" in JETS 22/3* (September 1979), 235-256.

[67] Ibid. 235-270.

[68] Is ceasationism the reformed view? page one.

[69] A Report on the Commission on the Theology and Church relations of the Lutheran Church- Missouri Synod, April, 1977, Condordia Publishing house, in the preface.

[70] Ibid.

wengine wameishia kushitakiwa mahakamani. Baadhi walipoona hawakufanikiwa katika maombi wamekata tamaa kwa kudhani hawana imani au Mungu hayuko pamoja nao.

Tatizo jingine ni baadhi ya wachungaji wa kilutheri nao kutekwa na mafundisho ya kipentekoste kiasi cha kupoteza jumla jumla utambulisho wao wa Kilutheri na Kiinjili. Changamoto ni namna ya kuhudumia wakristo wetu kiroho bila kupoteza utambulisho wetu, ushuhuda wetu na bila kwenda kinyume na Neno la Mungu.

Mahali pengine wachungaji na wainjilisti wamefuata mkumbo wa wakristo wao hata kama wenyewe watumishi hawaamini na kukubali kinachofanyika mtaani. Wanaheshimu washarika maana wana uwezo kifedha, wanachojali ni mkate wa kila siku na kwa hiyo wamekuwa Wachungaji wa mshahara ambapo liturgia na taratibu za kilutheri hazifuatwi. Namna ya kuomba ni watu wote kuomba kwa pamoja bila kuwa na kiongozi au kuomba mmoja baada ya mwingine, maombi ni ya kupayukapayuka yale **yanayozuiwa na Yesu katika Matayo**.

Hawa wamesahau kuwa Mungu hujua shida zetu hata kabla hatujaomba, anahudumia wema na wabaya, na kila tuombapo tunatazamia mapenzi ya Mungu yatimizwe na siyo yetu. La muhimu katika maombi ni kutambua kuwa maombi ni alama ya uhusiano na utegemezi wetu kwa Mungu tuwe tumepata au hatukupata, tunapata tukiwa na uhusiano na Mungu, tunakosa tukiwa na uhusiano na Mungu. Mfano mzuri ni Yesu aliyeomba Getsemane kikombe cha mateso na kifo kimuepuke. Ombi lake halikukubaliwa. Aliteswa na kufa. Hata hivyo alikuwa amesema kuwa mapenzi ya Mungu ndiyo yatimizwe. Alimlilia na kumlalamikia Mungu kuwa mbona amemuacha? Hapo hapo alimkabidhi Mungu Roho yake, “mikonini mwako naiweka Roho yangu”, anaiweka roho yake mikonioni mwa mtu aliyemuacha. Hii ni imani ya kumtegemea Mungu iliyo ya kiwangi cha hali ya juu.

Matatizo yanayokabili karama za roho mtakatifu ni pamoja na:

**(i) Ipo shida ya kufikiri kuwa kila ombi lazima lijibiwe**

- Hawa husahau kuwa Yesu mwenyewe aliomba kuepushwa kikombe cha mateso na kifo ila mapenzi ya Mungu yalikuwa Yesu ateswe na afe kwa ajili yetu.
- Wapo wanaoshindwa kufanikiwa wakajitenga na Mungu kwa kudhani kuwa Mungu hayuko pamoja nao. Wanashindwa kukumbuka kuwa Yesu aliyemlalamikia Mungu kuwa amemuacha (Mt. 27: 46) Yesu huyo huyo alimkabidhi Mungu Roho yake: “Mikononi mwako naiweka Roho yangu” (Lk 23: 46) ni imani kubwa kiasi gani, kufikia hatua ya kumkabidhi aliyekuacha Roho yako?
- Hawa wanasahau kuwa hata Paulo aliomba shida ya mwiba aishinde ila shida ya mwiba haikuisha bali alipewa tu uwezo wa kustahimili (2 Kor. 12: 19).
- Hawa wanashindwa kuelewa kuwa Mungu hudhihirika hata katika udhaifu wetu (Yohana 9: 1 - 3).

**(ii) Ipo shida ya wakristo wetu kutojiombea wenyewe na kuombea wengine**

Wakristo wetu wamekuwa tegemezi, hawapendi kujiombea na kuombea wengine, bali hutegemea wengine wawaombee wakati kila mkristo ni kuhani wa nafsi yake bila kutegemea wengine. Mahali pengine mtumishi wa kanisa letu alipoitwa kuombea mgonjwa alisema huyu kwa hali yake apelekwe kwa wapentekoste, alionesha kuwa hafai kabisa na alijidhalilisha maana hakufanya chochote kuombea mgonjwa. Tunaonesha ushuhuda gani kama hatuwezi kuhudumia wagonjwa kwa kiwango na taratibu zetu. Mchungaji Alex Kasisi katika semina za kiroho kuhusu maombi anaona matatizo yafuatayo:

- Wengine wameshindwa kuomba kwa kuhofia kutoweza mbwembwe za wengine katika maombi
- Wengine wanaoomba wanadharau wenzao wasioweza kuomba na hivyo kujiona wako juu kama farisayo
- Wengine huomba kwa kubadili sauti zao, wanaigiza sauti za wengine, n.k.
- Wengine huomba kwa kusukuma kuta kipindi cha maombi kinapofika na wengine hulia kila wanapoomba, kuna haja gani ya kulia kama unaombea maji ya kunywa?
- Wengine wamezama katika maombi wakasahau kuwa kuna kutafuta na kubisha: "Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni mtaona, bisheni nanyi mtafunguliwa". Kuomba kusiondoe kutafuta na kutafuta kusiondoe kuomba na kubisha hodi.

**(iii) Ipo shida ya kunena kwa lugha bila kufuata mwongozo wa Kibiblia**

Biblia inasema kuwa kunena kwa lugha kuongozwe na kanuni zifuatazo:
- Kunena kwa lugha kuambatane na kutafsiri yanayonenwa (1 Kor. 14:10-16)
- wanene wawili au watatu tena kwa zamu (1 Kor. 14:26-30).
- kuongea yanayoeleweka ni bora kuliko kunena kwa lugha (1 Kor. 14:1-9)
- Kunena kwa lugha ni muhimu kwa wasioamini bali walio na imani huhitaji Neno linaloeleweka.(1 Kor. 14: 22).
- kama hakuna wa kutafsiri yanayonenwa basi anayenena na anyamaze (1Kor. 14: 28)

**(v) Shida ya unabii kutumiwa kwa faida ya mtu binafsi**

Wengi wametumia njia hii kushawishi watu ili wanayopenda yafanzike, yafanzike haraka kwa kuwa yatadhaniwa kuwa Neno toka kwa Mungu. Wengi wanatumia njia ya unabii kushawishi kuoa mke anayetaka kumuoa. Hivi karibuni ilipita meseji ya mtu aliyetumia unabii kushawishi mke amkubalie, mke alisema wazi shida zake kabla ya kukubali kuwa ameachwa na wanaume 7, ametoa mimba 8 na mwishowe kuwa ameathirika kwa UKIMWI ndipo mwanamume akasema 'wala sikuwa na unabii, ndoa haiwezi kuwepo'.

Tusipokuwa macho yatatokea yaliyotokea Uganda mwaka 2000 ambapo Joseph Kibwetere aliwaambia waumini wake kuwa amefunuliwa kuwa mwisho wa dunia ni 2000. Aliwaambia wauze mali zao, mifugo, mashamba na nyumba waje kanisani Kanungu wasubiri kunyakuliwa. Na aliyasema hayo wakati Yesu mwenyewe alisema hajui siku wala saa ya kurudi kwake, lakini Kibwetere alijua ujio wa pili wa Yesu.

Baada ya miezi mitatu kupita waumini walianza kujihoji wataishije bila mali zao. Ndipo Kibwetere aliamua kuwaua waumini 1,000 kanisani kwa petroli. Anatafutwa na polisi haifahamiki kama aliuawa au alitoroka. Baba yake anajuta kwa nini alimzaa Kibwetere. Na mtoto wake alihuzunika kiasi cha kusema akimuona baba yake angemuua akiwa wa kwanza kwa aibu aliyoletea familia.

### 4.3 Mambo ya kuzingatia juu ya karama za Roho Mtakatifu

#### 4.3.1 Karama za Roho Mtakatifu si uhakikisho wa wokovu

- Wapo wanaodhani kuwa wasipokuwa na karama za Roho Mtakatifu basi hawana uhakika wa wokovu na pengine hufikri kuwa hawana imani. Neno la Mungu linasema wapo watakaojitetea kuwa walitoa mapepo kwa jina la Yesu lakini Yesu atawaambia waende motoni hawajui (Matayo 7:22).

- Katika Luka 10: 17-20 Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa wasifurahie mapepo kuwatii na miujiza kutendeka bali wafurahi kama majina yao yameandikwa mbinguni.[71]

#### 4.3.2 Uzoefu wa kiroho na hisia visiondoe umuhimu wa neno na sakramenti

Uzoefu wa mtu binafsi katika mambo ya kiroho haupashwi kuondoa umuhimu wa Neno la Injili ambalo liko huru na wazi kwa wote badala ya kukazia hisia za mtu binafsi ambazo huleta kujisifu au kusononeka na kukata tamaa.[72]

#### 4.3.3 Miujiza na ishara siyo uhakikisho wa kuwa na Roho Mtakatifu ndani yetu.

Mungu anaweza kuamua kutenda miujiza ndani ya kanisa lake hata sasa kama ilivyokuwa mwanzo, hata hivyo, Biblia hutuonya mara kwa mara dhidi ya kutekwa na mawazo ya miujiza tukasahau jambo muhimu la kuhubiri Injili. Ndiyo maana Yesu anatoa tahadhari dhidi ya watakaopendelea miujiza wakapotea na kupoteza hata wateule wa Mungu (Mat. 24: 24). Biblia inazuia kizazi hiki kudai miujiza ili kuamini (Mat. 16: 4). Wengine watasema tulitoa pepo kwa jina lako lakini Yesu atasema siwatambui, nendeni motoni ambapo kutakuwepo kulia na kusaga meno (Mat. 7:21-23).[73]

#### 4.3.4 Imani si lazima iondoe ugonjwa au matatizo

Walutheri huamini na kukubali kuwa magonjwa, maumivu, matatizo na vifo vipo duniani kama tokeo la anguko la mwanadamu. Yesu amekuja kutuokoa japo hili halimaanishi kuwa matatizo yameisha. Kwa mujibu wa Waebrania 12: 2 na 2Kor. 12: 7 matatizo ni kazi ya Mungu kwa ajili ya lengo jema. Pamoja na kuomba mtu atambue kuwa hawezi kumrubuni Mungu kwa maombi yake habari ya maisha na kifo chake, ndiyo maana kila mara maombi yanasisitiza kuwa mapenzi ya Mungu yatimizwe.[74]

#### 4.3.5 Karama zisiondoe umuhimu wa Ubatizo na Chakula cha Bwana

Ubatizo hutupatia baraka na agano la wokovu ambapo tunakumbushwa kutubu mara kwa mara ili Adamu wa kale afe tutakaswe na kupokea msamaha wa dhambi kila siku. Aidha, wakristo wakumbeshwe mara kwa mara umuhimu wa Chakula cha Bwana katika kutuhuisha upya katika maisha ya ufuasi na kutupatia baraka za kiroho badala ya kutegemea baraka za kunena kwa lugha na uponyaji[75] wakati huduma hizi si vyombo vya neema, ni huduma ya muda mfupi mfupi, kwani ukipona leo bado kesho utaugua na kufa. Hivyo, la muhimu ni vyombo vya neema vinavyotupa msukumo wa toba na ondoleo la dhambi tunapomtazama Kristo alivyojitoa kama sadaka na mtoa sadaka, mara moja na kwa ajili ya wote.

#### 4.3.6 Umuhimu wa kufundisha wakristo Neno la Mungu kwa miwani na tafsiri ya Kilutheri ili kulinda umoja, utambulisho na ushuhuda wetu

Aidha, ipo haja ya Wachungaji na viongozi wa Kanisa kufundisha Wakristo juu ya kazi za Roho Mtakatifu na Karama zake ili wafahamu vizuri Neno la Mungu wasiwe watu wa kuyumbishwa na kusema kila mara: ‘tena kweli’ kwa kila wanaloambiwa.

Tuwe mstari wa mbele kutembelea wagonjwa, tuwe na mikutano mikubwa ya kiroho na mahubiri ya hadhara kwa mpango maalumu, angalau kila usharika au mtaa mara 3 kwa mwaka, tujali na kutembelea wazee na wasiojweza, tuhusishe walei katika huduma za kanisa na uongozi maana kama Jesse Mugambi asemavyo, makanisa ya Afrika yanakua kwa kasi

---
[71] *Areport on the Commission,* 6-15.
[72] **Ibid.**
[73] Ibid
[74] Ibid
[75] Ibid,

kwa sababu ya kutumia walei kwa wingi ambao wako karibu na watu wakiwaongoza na kutatua shida zao huku wakiwa na uzoefu na taaluma anwai.[76]

Liturgia zetu na taratibu zetu za ibada zinaweza kuboreshwa na kuvutia wengi kwa njia ya ibada zenye kwaya zinazoimba kwa vifaa vya muziki na zinazoimba bila vifaa vya muziki na hapo kuleta vionjo mbalimbali ya kuvuta washarika. Vilevile, wenye umeme makanisani watumie vipaza sauti badala ya kutosikika wakati makanisa jirani ya kipentekoste yanasikika kwa vishindo wanapotumia fursa za teknolojia.

Aidha mahubiri yetu yaguse mahitaji na mioyo ya watu. Mahubiri yetu yasitekwe na mafafanuzi kana kwamba tuko chuo kikuu, mahubiri yetu yaepuke lugha ngumu za kifalsafa, yaepuke matumizi ya Kiyunani. Wakristo hawatazamii uwaambie unajua neno hili Wayunani wanaliita Anatos, au Arhe. Aidha, hawahitaji kujua kama aliyeandika waraka fulani anajulikana au hajulikani wala kujua kama mistali fulani ya Injili fulani inapingana na Injili nyingine. Hayo hayawasaidii kiimani badala yake huleta mashaka na kuondoka wakiwa hawana neno lililowasaidia. Vilevile tuwe na njia nzuri ya kufundisha wakristo wetu bila kuwakaripia wala kugombana nao maana uzoefu wa kanisa la Kilutheri nchini Marekani umeonesha kuwa makanisa yanayowasiliana vibaya na wakristo wenye matatizo hupoteza wakristo hao na mahali wanapowafundisha kwa upendo bila magomvi, wakristo hao wamebarikiwa na kukaa katika madhehebu yao ya kilutheri. Mabadaliko au mafundisho ya kuwarudisha yasiwe ya ghafla, bali yaingie polepole bila kuwahudhi.[77]

Kwa kuwa wanakarizimatiki wako tofauti sana, tusiwaweke wote katika kapu moja. Wapo wenye misimamo ya kawaida na wapo wenye misimamo mikali. Aidha tujue kuwa wengi wamefuata makanisa ya karama kwa sababu mbalimbali. Wengine ni kwa sababu za kutoelewana makanisani, kukosa uhakika wa wokovu, kukosa kujua uwepo wa Mungu wakati wa shida zao, kukosa mafanikio binafsi katika maisha, magonjwa, madawa ya kulevya, shida za kifamilia na shida katika dayosisi, majimbo na sharika zao.[78]

Wakristo wetu wasome Neno la Mungu kama linavyotafsiriwa Kilutheri badala ya tafsiri za kipentekoste. Na hapa tuwe na vitabu vidogovidogo vinavyojibu changamoto za upentekoste kwa miwani ya Kilutheri. Jambo zuri toka mahali popote lijadiliwe kwenye vikao vya Wachungaji na vikao vya Kanisa vya kikatiba ili kama ni jambo zuri tukubaliane sote, lisifanyike usharika huu wakati usharika mwingine haulijui. Hapo tutatunza umoja wa dayosisi na kanisa kwa ujumla.

Wachungaji na Wainjilisti wajulishwe hatari ya kuhusiana na watu wenye ushawishi wa kipentekoste. Wakristo wajulishwe shida ya ubatizo wa Roho Mtakatifu inavyoondoa mkazo wa sakramenti ya ubatizo. Angalia kwa makini maana ya ubatizo na chakula cha Bwana katika madhehebu ya kipentekoste na ukumbuke kuwa ulutheri unatahadharisha dhidi ya uzoefu binafsi wa ndani kiroho upingao umuhimu wa Neno na Sakramenti.

Aidha, uwe mwangalifu dhidi ya mikazo ya uponyaji, unenaji kwa lugha, unabii na utabiri jinsi mambo haya yanavyoweza kuwaondoa watu kwenye toba na msamaha wa dhambi.[79]

---

[76] Ibid.
[77] Ibid.12.
[78] Ibid, 13.
[79] Ibid.

Tufundishe Shule za Jumapili, Kipaimara na Elimu ya Kikristo mashuleni na vyuoni la sivyo watayumbishwa na kupotoshwa na madhara kwa kanisa na jamii yatakuwa makubwa. Maneno ya marehemu Askofu Henry Okulu yana maana kubwa anaposema kuwa ukiona mtuhumiwa mbele ya Hakimu ujue kuwa anawakilisha:

- Wazazi wake ambao wangefanya kitu fulani kabla ya tatizo kutokea
- Shule yake na walimu wake maana kabla ya tatizo hili wangekuwa wamefanya kitu cha kuzuia shida iliyotokea
- Kanisa lake ambalo kwa njia ya mahubiri, elimu ya kikristo na diakonia lingekuwa limefanya kitu fulani kuzuia tatizo lililotokea
- Serikali inayomhukumu maana nayo ingeweza kufanya kitu fulani kuokoa maisha ya mtuhumiwa huyu.

### 4.3.7 Umuhimu wa kufundisha Shule za Jumapili na Elimu ya Kikristo Mashuleni

- Ipo haja ya kufundisha shule za Jumapili
- Elimu ya Kikristo mashuleni
- Kipaimara
- Kwa njia hiyo tutakuwa tumewalinda watoto wetu dhidi ya changamoto za kuyumbishwayumbishwa na kuhamahama wakibadili madhehebu kama nguo. Madhara ya kuhamahama ni makubwa maana wengine huzuiwa kwenda hospitali eti waombe tu, wengine huzuiwa dawa za miti shamba wakati kwa mujibu wa Ezekiel 47:12 Mungu ameweka mitishamba na mimea kwa ujumla itubu wanadamu. Baya ni kutumia dawa hizo kishirikina.
- Wajibu wa malezi ni wa wazazi, shule kanisa na serikali kwa ujumla.
- Marehemu Askofu Henry Okulu anasema kuwa ukiona mtu amesimama mbele ya hakimu akijibu tuhuma fulani, ujue kuwa anawakilisha familia, shule, kanisa na serikali katika mahakama maana taasisi hizi zingefanya kitu fulani kabla ya shida kutokea.
- Katika malezi yetu tuhakikishe tunatoa tahadhari kwa watoto wetu wawe wana

Imetolewa na: **Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara** Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, KKKT aliyeongoza Somo la Biblia kuhusu **Neno Kuu.**
Kwa ajili ya **Mkutano wa Wachungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)**, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), 24 - 29 Septemba, 2016.